# تطهير الإعتقاد عن أدران الإلحاد

# KUSAFISHA KUWAAMINI UCHAFU WA KUTO AMINI

Kimeandikwa kwa kirabu na
SHEKH MOAMED ESMAEL AS SANANI
kime fisiriwa kwa kiswahili na
A.M. MSALLAM
KIZINGITINI
LAMU

KIME CAPISHWA NAKUIANGAZWA
WIZARAYA MAMBO ZA KISLAM NA WAKFU NA DA-WA
NA KUONGOZA.
WAKALA YA MAMBO ZA MACHAPISHO NAMATANGAZO
RIYADH
SAUDI ARABIA
1416 H. - 1995 G.

WAKFU YA MWENYEZI MUNGU

# تطهير الاعتقاد عن أدران الإلحاد

# KUSAFISHA KUWAAMINI UCHAFU WA KUTO AMINI

Kimeandikwa kwa kirabu na
SHEKH MOAMED ESMAEL AS SANANI
kime fisiriwa kwa kiswahili na
A.M. MSALLAM
KIZINGITINI
LAMU

KIME CAPISHWA NAKUIANGAZWA
WIZARAYA MAMBO ZA KISLAM NA WAKFU NA DA-WA
NA KUONGOZA.
WAKALA YA MAMBO ZA MACHAPISHO NAMATANGAZO
RIYADH
SAUDI ARABIA
**1416 H. - 1995 G.**

WAKFU YA MWENYEZI MUNGU

بسم الله الرحمن الرحيم


ح وزارة الشئون الإسلامية ، ١٤١٦ هـ

فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر

الصنعاني ، محمد إسماعيل

تطهير الاعتقاد .

٤٦ ص ، ١٢ × ١٧ سم

ردمك ٣-٤٣-٠-٢٩-٩٩٦٠

النص باللغة السواحلية

١- الإسلام - دفع مطاعن ٢- البدع في الإسلام ٣- التوحيد

أ- العنوان

ديوي ٢٤٠ ١٦/٠٦٥٩

رقم الإيداع : ١٦/٠٦٥٩

ردمك : ٣-٤٣-٠-٢٩-٩٩٦٠

١٤١٦هـ - ١٩٩٥م

# NENO LA MSAWAHILISHI

## KUPWEKESHA M'NGU

Dini mbali mbali zina afikiana kwenye:

1. Kuwa kuna M'ngu.
2. Kuwa M'ngu ni M'moja; Mwenye kuumba vitu vyote, mwenye kuvibakisha, na mwenye kutowesha.
3. Mambo fulani ya kumridhisha M'ngu ni lazima kuyafanya kwaajili ya M'ngu: mambo ambayo kuyafanya kunaitwa kuabudu.

Namna yakuabudu ndilo jambo lenye kuonyesha kuwa mwenye kuabudu mwenyewe anampwekesha M'ngu. au anamshirikisha! Na kabla hatujabaini haya kwa urefu, nivizuri kwanza tufahamu:-

NININI KUPWEKESHA M'NGU,
NA NININI KUSHIRIKISHA?

KUPWEKESHA M'NGU, ni kuamini kuwa M'ngu, ni m'moja pekeyake muumbaji, pekeyake mwenye kuruzuku, pekeyake mwenye kueka na kuondowa. kadhalika pekeyake mwenye kustahiki kuabudiwa! Amma kushirikisha M'ngu, ni kuamini kuwa M'ngu ana vyenye kumshiriki yeye katika kuumba au kupa rizki; au kukifanyia chochote lolote ambalo hafanyiwi asie kuwa M'ngu!

Dini zote za mbinguni zime baini, wazi katika maandishiyazo, upweke wa M'ngu. Na imani hii ya

kupwekesha, kwa hivyo, ndio imani yakiasli katika dini zamitume wote.

Amma Itikadi zenye kukhalifiana na imani hii bila ya shaka nikati ya mambo mageni yasio kufundishwa na mitume na ambayo yalipenyezwa na wafuasi wa dini hizo kwa sababu hii au nyengine! Kwenye mafundisho ya dini mbali mbali hata zile zenye ushiriki wazi, unaweza kuona vilevile namna zilivyo na ishara wazi zenye kukubaliana na imani ya kupwekesha:

Kwa mfano:

*Kwanza:* Mafundisho ya dini ya Zoroasta — mwalimu wa dini katika pashia kwenye Miaka 600 kabla ya kuzaliwa nabii Isa (A.S.). Ingawa mafundisho hayo yalidai kwamba huu ulimwengu Uliumbwa na nguvu mbili zikagawanyiana; lakini mafundisho hayo yanathibitisha kuwa nguvu ya shari khatimae itashindwa na nguvu ya kheri. Hili likiwa na maana yoyote litakuwa linaonyesha wazi kukubali kwa Zoroasta kwamba. Alieuumba ulimwengu ni m'moja nae niyule alie muita nguvu ya kheri, yenye kushinda, baada ya utesi mrefu, kati ya hio nguvu ya kheri, (ORMAZD) na nguvu ya shari, (ANGRAMAINYU).

Kwa sababu M'ngu haifai kushindwa. Na madamu amemthibitishia kushindwa, huwa amekwisha kumkanushia UM'ngu! Kadhalika mwito wa Zoroasta kwenye kuisaidia nguvu ya kheri dhidi ya nguvu ya Shari, unaweza kufasiriwa kama mwito wa kumuabudu M'ngu m'moja na kuyapenda yake, hali yakuchukia yenye kupingana na mapenziyake!

*Pili:* Pamoja na imani ya utatu (TRINITY) wanaoiamini wakristo, kitabu chao kitakatifu BIBLIA kwenye AGANO la kale na jipya, kina thibitisha wazi imani ya "KUPWEKESHA M'NGU".

Katika agano lakale:-

Mwanzo: 1:1 Pameandikwa:

"Hapo mwanzo M'ngu aliziumba mbingu na nchi"

vile vile agano la kale:

Kutoka: 20:3-5 Pameandikwa:

"Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijifanyie sanamu ya kuchonga wala mfano wa kitu chochote kilicho juu ya mbinguni wala chini ya duniani, wala kilicho majini chini ya duniani. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa Bwana Mungu wako ni Mungu mwenye wivu . . . ."

Kadhalika kwenye agano lakale:

KUMBU KUMBU LA TORAT: 6:4 Pameandikwa:

"Sikiza Ee Israeli; Bwana Mungu wetu, Bwana ndie mmoja".

Katika agano Jipya:

Yohana: 17:3 Pameandikwa:

Nauzima wa milele ndio huu; wa kujue wewe MUNGU WA PEKEE WA KWELI, NA YESU KRISTO ULIE MTUMA.

Na niwazi kuwa maana ya maneno haya ni kwamba: yesu alibaini wazi kuwa uzima wa milele, uko kwenye kujuwa M'ngu ni m'moja na kuwa yesu alitumwa tu kutoka kwake M'ngu wa pekee.

Ushiriki unaweza kupatikana kwenye imani ya mtu, lakini sio sana wenye kuenea. Ushiriki wenye kuenea, wenye kupatikana katika dini mbali mbali, ni ushiriki wa katika kuabudu. Sababu tunaweza kukumbuka kuwa; makafiri wa kiqurayshi katika zama za mtume Muham mad (S.A.W.) walikuwa wakikubali upweke wa M'ngu katika kuumba, kuruzuku, kuponesha, kufisha, na kuleta mvua, N.K. Lakini, walikuwa ni washiriki vile vile, kwa sababu ya kuwa na mambo ya kiibada ambayo walikuwa wakivifanyia vitu visio kuwa M'ngu!

Kitabu hichi, kilicho andikwa kwa lugha ya kiarabu na mwanachuoni mwenye kufuatwa mjuzi wa Elimu ya hadithi za Mtume (S.A.W.) Sheikh Muhammad Esmaei El-ameer-Elyamany Elssan-any, nikitabu chenye kumfundisha muislamu (imani yake safi kama alivyo takikana kuwa na imani hiyo na Kurani na hadithi zamtume Muhammad. Kitabu kina fundisha hayo kwa ushujaa wa mtu asie khofu kwa ajili ya M'ngu matayo ya mwenye kutaya.

Kwa sababu ya umuhimu wake sikushawiria kukiri kukisawahilisha nilipo ombwa kufanya hivyo na rafiki yangu mpenzi mpendwa kwa ajili ya M'ngu, mmoja katika wajumbe wa Saudi Arabia wa kufunza Uislamu Afrika Mashariki Sheikh SAYYID FATHAHUDHIN THANGAL BAQAWY M.A. AL-AZ-HAR, CAIRO. Nakunasihi msomaji ukisome kitabu hichi pasina kuwa na

fikra mbaya kinyume nacho kabla ya kukisoma sababu mwenye tabia hiyo hauoni kabisa mwangaza wahaki. Tabia hiyo ni ugonjwa wenye kumdiva mwenye nao kuijuwa kama anavyokosa kuona mwangaza wajuwa mgonjwa wamachol

*Mwisho Mola aumbao,*
*Asafishe masikio,*
*Mambo mema twambiwao,*
*Tujuwe pakulekeza,*

*Namuomba Himaliza,*
*Yawe mema kusikiza,*
*Tuweze kuyatimiza,*
*Juhudi zetu Rabana.*

*(Khatima) (Chozi la Damu) (Ubaitiwa) (20)*

بسم الله الرحمن الرحيم

Bismi Ilahi Rrahmani Rrahiim
Na yeye (MUNGU) Ndie Mwenye kutakwa msada

# UTANGULIZI

Namshukuru Mungu ambae hakubali upwekeshaji wa uola wake kutoka kwa waja wake, mpaka wa mkhusu kwa upwekeshaji wa Ibada, kumpwekesha vikamilifu, mbali na kumfanyia wendani; wasimfanyie mwendani wala wa simuombe pamoja naye yoyote, wala wasitegemee ila juu yake, wala wasikimbilie katika hali yoyote ila kwake, wala wasimuite ila kwa majina mema yake. wala wasijifikishe kwake kwa waombezi, (Ninani mwenye kuombea mbele yake pasina Idhniyake?? Na n'na amini kuwa: HAKUNA Mola ila MUNGU (mmoja) Mola mwenye kuabudiwa, na kwamba Muhammad ni Mja wake, na nimtume wake, ambae alimuamrisha aseme: (Sema sijimilikii manufaa wala madhara ila alilolitaka Mungu), Na Mungu atosha kuwa shahidi Mungu amrehemu yeye, najamaa wake, nawenye kumfuata yeye, katika kusalimika naaibu na kusafisha nyoyo, na (uchafu) wakuamini kila kitu kitiacho shaka.

Wabaadahu: Hiki ni: "kisafisho cha kuamini uchafu wakutoamini" kume nipasa kukitunga na kukanilazimu kukipanga, kwa ajili ya nilioyaona na nikayajua ya waja kufanya wendani (wa Mungu) katika miji navijiji na kila mahala; katika Yemeni, na Sham, na Misri, na Najdi, na Tihama, na katika majumba yote ya Kiislamu, nayo ni kuwa na Itikadi kwa makaburi. nawalio hayi, mwenye

kujidai kuwa na ujuzi wa mambo ya ghaibu na magunduo (ya kiajabu), na hali yeye ni katika wa ovu; haingii Msikiti wa Waislamu, na wala haonekani akirukuu kwa ajili ya Mungu, wala akisujudu, hajui Sunna wala Kurani wala hachi kufufuliwa wala hisabu.

Ikanipasa ni kanushe alilo lazimisha Mungu kulikanya. Wala nisiwe nikatika wenye kulificha alilo lazi misha Mungu kulidhirisha. Basi juwa kwamba hapa kuna misingi mingi ambayo nivikito vya dini, na nikati ya mambo muhimu ambayo kunapasa kuyajua juu ya wenye kupwekesha.

MSINGI WA KWANZA:

"Kila lilo kwenye Kur-ani ni haki"

Hakika kumejulikana katika lazima za dini:

Kwamba kila kilicho kwenye Kur-ani ni haki sibatili, ni kweli siurongo, niuongofu siupotevu, niujuzi siujinga, niyakini hakuna shaka ndani yake. Msingi huu ni msingi ambao hautimu uislamu wa yoyote wala imani yake ila kwa kuukiri, na hili ni jambo lilo kubaliwa. nahakuna ndani yake.

MSINGI WA PILI:

"Mitume walıletwa kuwaita watu kwenye kupwekesha Mungu kwa kupwekesha Ibada"

Hakika mitume wa Mungu — tangu wa kwanza wao mpaka wamwisho wao: walitumwa kwa ajili ya

kuwaita waja kwenye kumpwekesha Mungu kwa kumpwekeshea IBADA. Nakila mtume jambo lakwanza alilobishia hodi masikio ya watu wake, nikuwaambia (Enyi watu muabuduni Mungu hamna Mungu asie kuwa yeye) (Kwamba musiabudu ila MUNGU (mmoja) (Kwamba mumuabudu MUNGU na mumuogope namunitii mimi).

Na hili ndilo lililo bebwa na neno la: "LA ILAHA ILLA LLAHU". Hakika mitume waliwaita watu wao, kwenye kulisema neno hili nakuliamini, sio kulinena tu kwa ulimi. Na maana ya neno hilo, ni kumpwekesha MUNGU kwa uola na kwa IBADA, Na kukikanya chenye kuabubudiwa kisicho kuwa yeye na kujikenga nacho.

Na asli hii haina mapingano katika ililo libeba wala haina shaka, katika kuwa haitimu imani ya mtu yoyote mpaka aijue na aihakikishe.

MSINGI WA TATU:

"Vigawanyo vya kupwekesha"

Kupwekesha ni vigawanyo viili:

KIGAWANYO CHA KWANZA: Nikupwekesha uungu, na uumbaji, na upaji RIZKI.

Na maana yake ni kwamba, Mungu peke yake ndie muumbaji wa ulimwengu, na ndie mola wao na mpaji RIZKI wao.

Na hili hawalikanushi washirikishaji na wala hawamfanyii MUNGU, katikalo, mwendani, bali wao niwenye kulikiri hili kama itakavyo kuja katika MSINGI WAN'NE.

NA KIGAWANYO CHA PILI: Ni kupwekesha IBADA. Na maana yake, nikumukhusu Mungu peke yake kwa IBADA zote ambazo utakuja upambanufu wazo. Basi hili (la IBADA) ndilo wa lilo mfanyia Mungu wendani na neno "MWENDANI" lina shiria kumkiri Mungu mtukufu. Mitume walitumwa kulithubutisha la kwanza; na kuwaitawashirikishaji kwenye lapili, kama kusema kwao. Kuwambia washikishaji: "Je (kukhusu) Mungu kuna shaka, mwenye kuumba mbingu na ardhi? anawaita ili awaghufirie madhambi yenu" SURA: 14 aya 10.

> "Je kuna muumbaji asie kuwa MUNGU anae waruzuku mbinguni na nchini? Hakuna Mungu ila yeye . . . .

Na katika kuwakataza kushirikisha IBADA, SURA: 35 aya 3, Mungu amesema: "Na hakika tumelitumia. kila taifa, mtume" Kwamba muabuduni Mungu na mumuepuke shetani — SURA: 16 aya 36 yaani hali yakuyaambia mataifayao: "MUABUDUNI MUNGU" basi imeonyesha kwa kusema: "Katika kila taifa" kwamba mataifa yote hayakupelekwa mitume ila kwa sababu ya kuwataka kumpwekesheya (MUNGU) IBADA, sio kuwataka kujulisha kuwa Mungu ndie alie umba ulimwengu. nakwamba yeye ndie mola wa wambingu na n'chi. Kwani wao niwenye kulikiri hili; na kwa hivyo hazikuja aya kukhusu hili mara nyingi ila kwa temko la kuthibitisha: kama: (je kuna mwenye kuumba asie kuwa Mungu SURA: 35 Aya 3).

(Je kukhusu Mungu kuna shaka; muumbaji wambingu na ardhi?) SURA: 14 Aya 10.

(Je asie kuwa Mungu, nimfanye mtawala, muumbaji wa mbingu na ardhi) SURA: 6 Aya 14.

(Huku ni kuumba kwa Mungu, basi nionyesheni. kitugani wameumba wasio kuwa yeye) SURA: 31 Aya 11.

(Nionyesheni, kitu gani wameumba katika ardhi? Au wanaushirika mbinguni?

(Huku ni) kuuliza kikuwathibitishia wao kwa sababu wao ni wenye kulikiri hilo.

Nakwahivi utajua kuwa washirikishaji hawakufanya masanamu, wala hawa kuyaabudu, wala hawakumfanya masihi (ISSA) na mamake, wala hawakuwafanya Malaika, niwendani wa Mungu kwa kuwa wamewashirikisha wao katika uumbaji wambingu na ardhi! Bali wali wafanya wao (hivyo) kwa sababu ya kuwa wao wana wa kurubisha kwa Mungu, kama walivyosema: wao niwenye kumkiri Mungu kwenye yale yale maneno yao ya kufuru, na kwamba wao ni waombezi kwa Mungu!

Mwenye ezi Mungu amesema: (Nawanaabudu, asie kuwa Mungu visio wa dhuru wala kuwafaa na wanasema: *hawà ni waombezi wetu kwa Mungu. Sema munamueleza* Mungu asioyajua mbinguni wala ardhini? Kutakata ni kwake nakutukuka mbali na wanao mshirikisha: SURA 10 Aya 18.

Mungu amefanya, kule kufanya kwaowaombezi, ni SHIRKI na akajitakasa nayo, kwa sababu hatoombea. kwake yoyote pasina Idhni yake, vipi tena wanajithubutishia waombezi asio kuwaruhusu katika maombezi wala wasio kuwa wasawa nayo: wala wasio watosheleza na Mungu chochote?

MSINGI WA N'NE:

"Washirikishaji wanakiri kuwa Mungu ni muumbaji wao".

Hakika wa shirikishaji ambao Mwenye ezi Mungu alipeleka mitume kwao, ni wenye kukiri kwamba: M'ngu ni muumbaji wao.

"Na lau kama ungewauliza wao: Ninani aliewa umba? Wangesema: Ni M'ngu (SURA: 43 Aya 87).

Na kwamba yeye ndie alie umba mbingu na nchi:

"Na lau kama ungewauliza ninani alieumba mbingu na nchi? wangesema: ameziumbazo mwenye nguvu mjuzi" SURA: 9 Aya 43.

Na kwamba yeye ndie mwenye kuruzuku ambae anakitoa kilicho hayi kwenye kilicho kufa, na anakitoa kilicho kufa kwenye kilicho hayi; Na kwamba yeye ndie mwenye kupanga mambo mbinguni na ardhini. Na kwamba yeye ndie mwenye kumiliki masikizi na maangalizi na nyoyo.

"Sema ninani mwenye kuwaruzuku nyinyi kwenye mbingu na ardhi? au ni nani mwenye kumiliki masikizi na maangalizi? Na ninani mwenye kutoa kilicho hayi kwenye kilicho kufa? Na ninani mwenye kutoa kilicho kufa kwenye kilicho hayi? Na ninani mwenye kupanga mambo? Watasema: NI MUNGU, (BASI) Sema: (Je) hamuogopi?" SURA: 10 Aya 31.

"Sema: Ni yanani ardhi na walio ndani ikiwa mnajua? Watasema: Niya M'ngu. Sema: hamuwaidhiki? Sema ninani mola wa mbingu saba na mola wa arshitukufu? Watasema: Niza M'ngu. Sema: (Je) hamuogopi? Sema: ninani ulio mkononi mwake ufalme wa killa kitu nae anahifadhi wala hahifadhiwi, ikiwa mnajua? Watasema ni wa M'ngu: Sema (BASI) vipi mna danganywa? SURA: 23 Aya 84 - 89.

Na huundie Fir-auna, pamoja na kutopea kwake kwenye ukafiri, nakudai kwake madai maovu mno, na kutemka kwake neno bovu sena, anasema M'ngu kukhusu yeye, hali yakueleza khabari ya Musa (A.S.): "Hakika umejua (kuwa) hakuziteremsha (huja) hizi ila mola wa mbingu na nchi (hizi) ni dalili" SURA: 17 Aya 102.

Na alisema Iblisi: "Hakika mimi ninamuogopa M'ngu mola wa viumbe vyote" — SURA: 59 Aya 16.

Alisema tena: "Ewe mola wangu kwa sababu ya kunipoteza, . . . ." SURA: 17 Aya 39.

Alisema tena: "Ewe mola wangu nipa muhula' (SURA: 15 Aya 36) . . . . Nakilla mshirikishaji ni mwenye kukiri kwamba M'ngu ndie muumbaji wake, na muumbaji wa mbingu na nchi, na ndie mola wazo na ndie mola wa zilizomo ndani yazo na ndie mwenye kuwaruzuku wao. Nakwahivyo waliwatolea huja mitume kwa kuwaambia: "(Je) Mwenye kuumba ni kama asie umba?" SURA: 16 Aya 17. Na kwa kuwaambia: "Hakika mnao waomba wasio kuwa M'ngu hawatoumba nzi na hata kama wangekusanyika kwa (AJILI) ya hilo, SURA: 23 Aya 73.

Na washirikishaji wote niwenye kulikiri hilo hawalikanushi.

## MSINGI WA TANO:

"Msingi wa Ibada ni kumpwekesha M'ngu".

Hakika Ibada ni upeo wa mlango wa kunyenyekea na kujidhalilisha, na wala halikutumiwa (neno hili) ila kwa kumnyenyekea M'ngu, kwa sababu yeye ndie mwenye kupa neema kubwa. Na kwa hilo ame kuwa mwenye haki ya mwisho wa upeo wa kunyenyekewa kama ilivyo katika (kitabu Al kashaf). Kisha, hakika kichwa cha ibada na msingi wake ni kupwekesha (Ibada) kwa ajili ya M'ngu, ambako kunafahamishwa na neno lake ambalo mitume wote wameita kwenye neno hilo: Nalo ni neno la "LA ILAHA ILLA LLAHU" — (Hakuna Mungu Illa (Allahu).

Namakusudiwa ni kuitakidi maana yake, na kufanya kulingana na litakavyo, sio kulisema kwa ulimitu. Na maana yake: Nikumpwekesha M'ngu kwa ibada na kwa uola, na kumkanusha yoyote, na kuwa mbali na yoyote mwenye kuabudiwa asie kuwa yeye. Na hakika makafiri waliyajua maana haya, kwa sababu ndio wenye lugha ya kiarabu, wakasema: "(Je) amewafanya waungu ni M'ngu mmoja? Hakika hili ni jambo laajabu" — SURA: 38 Aya 5.

## SAMPULI ZA IBADA:

Baada ya kufahamu misingi juwa kwamba M'ngu ameifanya ibada kuwa na sampuli nyingi:-

A: ZAKIKUAMINI: Nahizo ndizo msingi wa ibada, nako nikuamini kuwa M'ngu ndie mola wa pekee ambae ndie mwenye kuumba na (mwenye) killa jambo, na nimiliki yake kufaa na kudhuru, nakwamba yeye ndie ambae hana mshirika wake, wala haombei mbele yake yoyote ila kwa idhni yake, na kwamba hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki asie kuwa yeye, na yasio kuwa hayo katika yenye kulazimiana na uola.

B. ZAKIMATEMSHI: Nako ni kutemka neno la kupwekesha, kwani mwenye kuamini yalitajwa na wala siyatemke, haihifadhi damu yake wala mali yake na huwa ni kama Iblisi kwani yeye anaamini umoja wa M'ngu kamwe anaukiri kama tulivyo tangulia kumsema, isipokuwa yeye hakufuata amri ya M'ngu kwa hivyo akawa kafiri. Na mwenye kutemka na asiamini anaihifadhi damu yake na mali yake na hisabu yake iko juu ya M'ngu, na hukmu yake ni hukmu ya wanafiki.

C. ZAKIMUILI: Kama kusimama, na kurukuu, na kusujudu katika swala. Na nikatika hizo: kufunga, na 'kazi zahija, na kutufu.

D. ZAKI MALI: Kama kutoa fungu la mali, kwa kufuata alililoliamrisha M'ngu; nasampuli za wajibu, na yenye kupendekezwa kwenye mali na miili na vitendo, ni nyingi sana lakini hizi ndizo muhimu!

## "MITUME WALI TUMWA KWA AJILI YA KUITA KWENYE KUMPWEKESHA M'NGU KWA IBADA"

Na yakisha kuthubutu mambo haya, jua kwamba M'ngu amewatuma mitume, (A.S.) tangu wamwanzo

wao mpaka wa mwisho wao, kuwaita watu kwenye kumpwekesha M'ngu kwa Ibada, sio kwenye kuthubutisha kuwa yeye M'ngu amewaumba wao, na kama hilo, sababu wao ni wenye kulikiri hilo, kama tulivyo thibitisha na tukakariri.

Na kwa hivyo walisema: "Je) Ume tujilia sisi ili tumuabudu M'ngu peke yake?" SURA: 7 Aya 69 yaani (ume tujilia) ili tumpwekeshee yeye ibada na tumukhusu yeye kwa hio ibada pasina waungu wetu? Kwa hivyo hawakukataa isipo kuwa la mtume kutaka kwao kupwekesha ibada kwa M'ngu.

Na wala hawa kumkanya M'ngu, na wala hawakusema: yeye M'ngu haabudiwi, kamwe walikiri kuwa yeye anaabudiwa, na wakakanusha kuwa yeye ni wakupwekeshewa Ibada. Kwa hivyo wakaabudu pamoja na M'ngu asiekuwa yeye, na wakamshirikisha pamoja na yeye asiekuwa yeye, na wakamfanyia yeye wendani, kama M'ngu alivyo sema:

> "Musimfanyieni M'ngu wendani na hali mnajua". SURA: 2 Aya 22.

Yaani na hali nyinyi mnajua kuwa hana mwendani.

Na walikuwa wakisema kwenye (talbiya) (kuitikia) kwao kwaajili ya hija: "Tuna kuitika huna mshirika ila alie wako mshirika, unaemmiliki na asiemiliki".

Na alikuwa mtume akiwasikia wakinena: "LA SHARIKA LAKA" — "HUNA MSHIRIKA" akisema (Mtume): "Hakika wangekuwa wamempwekesha (alie tukuka utukufu wake) lau kama wangewacha kusema kwao: (ISIPOKUWA ALIE WAKO MSHIRIKA).

Kwa hivyo kulekule kushirikisha kwao M'ngu ndiko kumkiri kwao M'ngu.

M'ngu amesema: "WAKOWAPI WASHIRIKISHWA-WENU AMBAO MLIKUWA MKIDAI (kuwa wao niwashirika wa M'ngu) SURA: 6 Aya 22.

"Nakutasemwa: waiteni washirikishwa wenu wakawaita na wasiwaitikie" SURA: 28 Aya 4.

"Sema waiteni washirikishwa wenu kisha mnichimbie na msinipe mda" SURA: 7 Aya 194.

Kwa hivyo kulekule kufanya wendani, ni kumkiri M'ngu. Na wala hawakuwaabudu wenye kushirikishwa. kwa kuwa nyenyekea na kwakujikurubisha, kwa kuwaekea nadhri nakuwachinjia ila kwa kuitakidi kwao kwamba: hao wenye kushirikishwa wanawakurubisha wao kwa M'ngu nawatawaombea wao kwake. Kwa hivyo M'ngu akawatuma mitume waamrishe kuwachwa Ibada ya chochote kisicho kuwa yeye, na wabayini kwamba itikadi hii ambayo wanaitakidi kwa washirikishwa ni batili, na kwamba kujikurubisha kwao ni batili, na kwamba haliwi ila kwa M'ngu peke yake na huku ndiko kupwekesha ibada. Na walikuwa ni wenye kukiri — kama ulivyo juwa katika msingi wanne — upwekeshaji wa uola, nao ni kwamba M'ngu ndie muumbaji peke yake na mwenye kuruzuku peke yake.

Na kwahili utajua kwamba upwekeshaji ambao mitume waliwaitia wao, tangu wa mwanzo wao nae ni Nuhu (A.S.) — mpaka wa mwisho wao nae ni Muhammad (S.A.W.) — niupwekeshaji wa ibada. Na kwa

hivyo mitume walikuwa wakiwaambia wao: "KWAMBA MSIABUDU ASIE KUWA ALLAH" "MUABUDUNI MUNGU HAMNA MUNGU ASIE KUWA YEYE".

Na hakika walikuwa miongoni mwa washirikishaji wenye kuabudu malaika,. na wakiwalingania wao WAKATI wamashida. Na wenye kuabudu mawe na wakiyaomba kwenye magumu; kwa hivyo mwenye ezi M'ngu akamtuma Muhammad (S.A.W.) awaite wao kwenye kumuabudu M'ngu peke yake, wampwekeshee yeye ibada kama walivyo mpwekeshea uola — yaani uola wambingu nan'chi. Na wampwekeshe juu ya maana ya maongozi ya neno la: "LAILAHA ILLALLAHU" hali ya kuamini maana yake na kufanya kulingana na maelekezwa yake, na wasimlinganie pamoja nayeye yoyote. Na mwenyeezi M'ngu amesema: Ana yeye ulinganizi wajibu wao kwa chochote. "SURA: 14 Aya 14. Na wahaki na ambao mnawalingania wasiokuwa yeye hawa-M'ngu amesema: "Na juu ya M'ngu tegemeani mkiwa niwaumini" SURA: 5 Aya 22. Yaani, ni katika sharti ya ukweli katika kumuamini M'ngu, kutotegemea ila juu yake, nawampwekeshe yeye kwa tawakul: kama inavyo kumpwekesha yeye kwa dua, na kuomba msamaha.

Na M'ngu amewaamrisha waja wake waseme: "IYYAKA NA'BUDU" peke yako tunakuabudu, wala hawi mkweli mwenye kunena hili mpaka ampwekeshee M'ngu ibada, na ikitokuwahivyo atakuwa mrongo, mwenye kukanywa kunena neno hili; kwa sababu maana yake ni: tuna kukhusu wewe kwa Ibada, na tunakupwekesha wewe kwayo pasina yoyote.

Nayo ndiyo maana ya kusema kwake: "Peke yangu niabuduni" SURA: 29 Aya 56. NA: "Peke yangu niogo-

peni" SURA: 2 Aya 14. Kama inavyo julikana katika Elmu ya Bayani; kutanguliza ambacho haki yake nikucheleweshwa kuna maanisha kukhusu, yaani Msimuabudu ila M'ngu wala msimuabudu asie kuwa yeye, wala msimuogope asiekuwa yeye, kama ilivyo kwenye (Kashaf). Kumpwekesha M'ngu kwa kumpwekeshea Ibada hakutimu ila maombi yote yawe nikwake, na kuita kwenye mashida na raha hakuwi ila kwa M'ngu peke yake, na kuomba msada kuwe kwa M'ngu peke yake. Nakutegemea kuwe kwa M'ngu, na nadhiri nakuchinja kuwe ni kwa ajili ya M'ngu, na sampuli zote za ibada: kunyenyekea, na kusimama kwa kujidhalilisha kuwe ni kwa ajili ya M'ngu, na kurukuu na kusujudu na kutufu na kujitoa nguo na kunyoa na kupunguza nywele (KUBIRA) yote yasiwe ila kwa ajili ya M'ngu mtukufu.

Na mwenye kufanya lolote katika hayo kwa ajili ya kiumbe hayi au maiti au kisicho kuwa naroho au chochote, huwa ameshirikisha katika ibada. Na huwa mwenye kufanyiwa mambo hayo ni M'ngu wa wenye kumuabudu yeye, ni sawa awe malaika au mtume, au waliyi, au mti, au kaburi, au jini au hayi au maiti; na huwa, mwenye kuabudu kwa ibada hii yaani kwa sampuli yoyote ya hizo, ni mwenye kukiabudu kiumbe kile tena mwenye kumshirikisha M'ngu, na angamkiri M'ngu na angamuabudu, kwani kukiri, kwa washirikishaji, M'ngu na kujikurubisha kwao kwake hakukuwatowa nje ya (shirki) na (nje) ya kupasa kumwaga damu zao na kuchukuwa watoto wao mateka na kuchukuwa mali yao hali yakuwa ni ghanima ya Waislamu.

Mwenye ezi M'ngu amesema: "Mimi ni mwenye kujitosha mno wa washirika na shirki" wala M'ngu haku-

bali ibada yoyote alio shirikishwa katikayo yoyote asiekuwa yeye" Wala hamwamini yeye alie muabudu pamoja na yeye mwengine.

Kumkiri M'ngu hakutoshi katika kupwekesha. Likisha kuthibitikia kwamba washirikisha kwao wendani katika viumbe kwenye ibada, wala (kukiri kwao) hakukuwatoshelezea chochote na M'ngu, na kwamba kuwaabudu hao ni kule kuitakidi kwao juu ya hao, kwamba wanadhuru na wananufaisha na kwamba wao wanawakurubisha wao, — na kwamba wao watawaombea wao kwa M'ngu, kwa hivyo wakawachinjia vichinjwa, na wakawafanyia TWAWAF, na wakawawekea nadhiri, na wakasimama hali ya kujidhalilisha, wanyenyekevu kwa ajili ya kuwatumika wao, na wakawasujudia. Na pamoja na haya yote wao ni wenye kumkiria M'ngu uola na kwamba yeye ndie Muumbaji, lakini wao waliposhirikisha na wala hakukuhisabiwa kukiri kwao huku kwa sababu vitendo vyao vimekukanusha. Kwa hivyo hakukuwafaa wao kukiri upeke wauola. Kwani kaida ya Mwenye kumkiri M'ngu kwa kumpwekeshea uola; ni ampwekeshe yeye kwa kumpwekeshea ibada, akitofanya hivyo, kukiri kwa kwanza kutakuwa batili, na hakika watajua hilo hali nao wako juu ya mitabaka ya moto na watasema: "Tuna apa kwamba hakika tulikuwa kwenye upotevu wazi tulipokuwa tukiwalinganisha nyinyi na mola wa viumbe vyote. SURA: 26 Aya: 97-98.

Pamoja na kwamba wao hawakuwalinganisha wao na yeye kwa killa upande; hawaku wafanyawao ni waumbaji, wala ni wapajirizki, lakini wao walijua na haliwako ndani yaukeo wajahannam kwamba kuchanganya, kwao kukiri, na chembe moja kati ya chembe

za shirki katika kuipwekesha Ibada, kumewafanya wao nikama aliewafanya masanamu ni sawa na mola wa yiumbe!

MUNGU amesema: "Nawala hawaamini wengi wao. MUNGU, ila huwa ni washirikishaji" yaani "hawakiri wengi wao, katika kumkiri Mungu, na katika kwamba yeye amewaumba wao na ameumba mbingu na ardhi ila na wao huwa ni washirikishaji kwa kuabudu masanamu. Kamwe Mungu ameiita. Riya katika twaa (SHIRKI) pamoja na kwamba mwenye kufanya twaa, hakumkusudia kwayo asie kuwa MUNGU MTUKUFU, na hakika tu ametaka daraja kwa hiyo twaa katika nyoyo za watu Mwenye riya huwa amemuabudu Mungu sio asie kuwa yeye, lakini yeye amechanganya Ibada yake na kutaka daraja katika nyoyo za watu, kwa hivyo hakukubaliwa ibada, na Mungu ameiita shirki kama alivyo pokea Muslim katika hadithi ya Abi hurayrah" (R.A.) amesema Mtume amesema (S.A.W.) "Anasema Mungu: Mimi nimwenye kujitosha mno na washirika na shirki" Mwenye kufanya amali na akamshirikisha katikayo pamoja nami asiekuwa mimi na muacha yeye na shirki yake".

Kamwe Mungu amekuita. kumpa (mtu) jina la 'Abdul-harithi (mja wa harith) shirki', kama alivyo sema Mungu: "Alipowapa wao mwema walimfanyia wendani katika aliowapa" — SURA: 7 Aya 190. Hakika amepokea Imamu Ahmed na Tirmidhy katika hadithi ya samrah kwamba mtume (S.A.W.) amesema: "alipochukua hawaa (mimba) na alikuwa hamponei mtoto alitembelewa na Iblisi na akamwambia hatopona mtoto wako mpaka umwite (Abdul — harith) hapo hawa akamuita (hivyo) na akapona. Na lilikuwa hilo ni katika wahyi

washetwani na amri yake. Hapo Mungu akateremsha aya hizo. Na akakuita kuita huku ni shirki na alikuwa Iblisi amejiita (Al-harith). Na kisa (hiki kiko katika (Kitabu) (Al-durril-manthuri) na kisichokuwa hiko.

"Kuitakidi asiekuwa Mungu ni shirki"

Hakika umejua kwa haya yote: kwamba mwenye kuitakidi mti au jiwe, au kaburi, au malaika, au jini, au alie hayi au maiti: kuwa (chochote katika hivyo) kinafaa au kinadhuru au kuwa kina kurubisha kwa Mungu, au kinaomba kwa Mungu katika haja yoyote kwenye haja za kilimwengu, kwa kujiombea kwacho tu, na kutawasali kwa Mungu — isipokuwa lililo kuja katika hadithi ambayo ina maneno katika kukhusu mtume Muhammad (S.A.W.) au kama hilo — hakika yeye huwa ameshirikisha pamoja na M'ngu mwengine, na huwa ameitakidi ambalo sihalali kuliitakidi, kama walivyoitakidi washirikishaji masanamul

Licha mwenye kueka nadhiri, kwa mali yake na mtoto wake, kwa maiti au kwa alie hayi, au akataka kwa maiti huo ambalo halitakwi ila kwa Mungu kwenye mahitaji: kama afiya ya mgonjwa wake, au kuja asiekuwako wake au kupata lolote katika matakwa yake, hakika hio ndio shiriki enyewe, ambayo walikuwa, au wako, juu yake wenye kuabudu masanamu.

Na kueka nadhri kwa mali juu ya maiti na kama yeye (maiti) na kuchinja (mnyama) juu ya kaburi, na kutawasali kwalo, na kutaka mahitaji kwalo, ndilo hasa walilokuwa wakilifanya (watu wazama za jahiliya. Isipokuwa walikuwa wakiwafanyia walio waita masanamu. Na watu wa makaburi wamemfanyia wanaemuita waliyi

na kaburi, na mash-had, na majina hayana athari yoyote wala hayabadilishi maana kwa dharura ya kilugha, na ya kiakili, na ya kisharia. Kwani mwenye kunywa tembo na akaliita maji hawi amekunywa ila tembo, na mateso yake ni mateso ya mwenye kunywa tembo, na pengine yeye yatazidi mateso yake kwa ajili ya udanganyifu na urongo wa kuita.

Na hakika imethubutu kwenye hadithi kuwa — "Watakuja watu watakao kunywa tembo wakiliita kwa lisokuwa jina lake, na mtume amesema kweli; kwani yamekuja mapote ya watu wenye kunywa tembo na kuliita (NABIIDH). Na wakwanza aliekiita chenye hasira za Mungu na kumuasi yeye, kwa majina yenye kupendeza kwa wenye kusikia, ni IBLISI (Mungu amlaani)". Kwani yeye alimwambia baba wa viumbe (ADAM) (A.S.) "Ewe Adam sikuonyeshi mti wa maisha) ya kudumu na ufalme usio toweka?" SURA: 20 Aya 120. Kwa hivyo akauita, mti ambao Mungu amemkataza Adam kuukurubia, mti wa maisha ya kudumu, kwa ajili ya kuivuta tabia yake kwenye mti huo, na kwa ajili ya kutikisa bidii kwa ajili ya kuukurubia na kwa ajili ya kumdanganya yeye kwa jina alilolizua la mti huo, kama ambavyo ndugu zake wenye kumfuata yeye wanaiita bangi: (TONGE LA RAHA). Na kama ambavyo madhalimu wanaziita, wanazozipokea katika mali ya watu kwa dhulma (ADABU). Wana sema adabu ya kuuwa, adabu ya kuiba, adabu ya tuhuma, kwa kubadilisha jina la dhuluma kwa jina la adabu. Kama wanavyo badilisha baadhi ya vyenye kupokewa kwa jina la "Kunufaisha au uchungaji, na baadhi nyengine kwa jina la adabu ya vipimo na mizani. Na majina yote hayo, kwa Mungu, ni dhuluma na uadui kama anavyo jua yoyote alie nusa

harufu ya Kurani na Hadithi, na yote hayo yamechukuliwa kwa Iblis, alipouita mti ulio haramishwa, mti wa maisha ya kudumu. Na ni kama hivyo kuiita kaburi (MASH-HAD) na wenye kuitakidi kwa aliye ndani yake (WALIYI), hakuitowa nje ya jina la sanamu kwa sababu wao wanayafanyia hayo makaburi kama washirikishaji wanavyo wafanyia masanamu, na wanayatufu hayo makaburi kama mahujaji wanavotufu nyumba ya mwenye ezi M'ngu tukufu na wanayashika (kwa kuyatukuza) kama wanavyo shika mahujaji nguzo za Al-kaba, na wanasema na maiti kwa maneno ya ukafiri, kama kusema kwao: "JUU YA M'NGU NA JUU YAKO" na wanawaita katika mashida kwa majina yao na kama hayo, na kila taifa lina mtu linayemlingania.

Watu wa Iraki na India wanamlingania ABDUL-KADIRI I-JIYLY, Na watu wa majabali ya tihama wana katika kila mji maiti wanaemlingania kwa jina lake, wanasema "Ewe Zaylaii" "Ewe IBNUL-UJAYLI" Na watu wa Maka na TWAIF: "Ewe IBNUL-ABBAAS" Na watu wa Misri "Ewe RIFAAII" "Ewe BADAWY" Na watu wa YAMAN: "Ewe IBNU AL-WAN".

Na katika kila kijiji kuna maiti wanawaita na kuwalingania na kuwatarajia kwa ajili ya kuvuta kheri au kuondoa shari.

Na hivi ndivyo halisi walivyokuwa wakifanya washirikishaji masanamu; kama tulivyosema katika mashairi ya kinajdi:

*Kwayo wameyaregesha, ya suwaa na kamaye,*
*Yaghutha na wudi kisha, si wudi ya nipendae,*
*Kwenye ya kuhangaisha, wameita majinae.*
*Kwita ahitajiae, pekee muhitajiwa.*

*Maranyingi vichinjwao, wachinjiwa kwa juhudi,*
*Hachinjiwi M'nguwao, kwa ujinga na kusudi,*
*Niwangapi watufuo, makaburi maridadi,*
*Washika kwa taabudi, nguzo yalio jengewa.*

Akisema kuwa mimi nimechinja kwa ajili ya M'ngu tu nanimetaja jina la M'ngu juu yake mwambie ni kwa nini ulikikurubisha, unachokichinja, na mlango wa kaburi la unaemtukuza na kumuitakidi? Je ulikusudia kwa hilo kumtukuza? Akisema: ndio, Mwambie kuchinja huku basi ni kwa ajili ya asiekuwa M'ngu. Kamwe umeshirikisha na M'ngu asiekuwa yeye, na ukiwa hukukusudia kumtukuza je basi ulikusudia kuchafua mlango wa ziyara na kuwanajisi wenye kuigia huko? Wewe unajua kwa yakini: kuwa hukukusudia hivyo kabisa, wala hukutaka isipokuwa la kwanza na wala hukutoka nyumbani ila kwa ajili ya kumkusudia yeye, kisha ni hivyo hivyo kumuomba kwao.

Hili basi walilo nalo hawa nishirki pasina shaka!

Na pengine wanawaitakidi baadhi ya mafasiki walio hayi wakawaita kwenye shida na raha na hali wao wameyakalia mabaya na maovu, hafiki alipo waamrisha M'ngu wajawake kufika, hahudhurii (Swala) ya juma na wala ya jamaa, wala hamtembelei mgonjwa wala hasindikizi jeneza wala hachumi halali na anaengeza kwenye hilo kujidai kutawakali na ujuzi wa yalio ghibu, na Iblisi anamvutia yeye watu ambao (yeye Iblisi) amejenga vitundu katika nyoyo zao na amezaa ndani na ameangua, wana sadiki uzuzi wake na wanalitukuza jambo lake, na wanamfanya huyu mwendani wa Mola wa viumbe vyote na mfano wake, nazililia akili zimekwenda wapi, na zililia sharia zimekosa kujulikana vipi?

"Hakika ambao mnawalingania ni waja kama nyinyi" SURA: 7 Aya 154.

Ukisema je wanaweza kuwa, hawa wenye kuitakidi makaburi, na mawaliyi, na mafasiki, na wapuzi, ni washirikishaji, kama wenye kuyaitakidi masanamu? Nasema: Ndio, limepatikana kwao lilopatikana kwa wale, wakalingana na wao kwenye hilo, kamwe wamezidisha katika kuitakidi na kunyokea na kujidhalilisha; hapana tofauti kati yao.

Ukisema: hawa watu wa makaburi wanasema, sisi hatumshirikishi M'ngu na wala hatumfanyii mwendani, na kuwategemea mawaliyi si shirki.

Nasema: Ndio, wanasema kwa vinywa vyao yasiokuwako nyoyoni mwao, lakini huku nikutojua kwao maana ya shirki. Kwani kutukuza kwao mawaliyi na kuwachinjia vichinjwa ni shirki.

Na M'ngu amesema: "Sali kwa ajili ya mola wako na uchinje" yaani si kwaajili ya asiekuwa yeye, kama kunavyo onyeshwa na utangulizaji wa DHARF (katika lugha ya kiarabu). Na mwenye ezi M'ngu anasema: "Na kwamba Misikiti ni ya M'ngu msimlinganie pamoja na yeye yoyote. SURA: 72 Aya 18.

Na hakika umejua kwatulio yatanguliza hivi karibuni kwamba yeye Mtume (S.A.W.) aliita riya shirki, Je yatakuwa hali gani kwa tulioyasema? Basi haya wanao wafanyia mawaliyi wao; ndio yale yale walioyafanya washirikishaji na wakawa kwayo niwashirikishaji, wala hakuwafai wao kusema kwao: "Sisi hatum-

shirikishi M'ngu na chochote'' sababu vitendo vyao vimeyafanya maneno yao, kuwa ni urongo.

Ukisema: ''Wao hawajui kuwa wao ni washirki kwa wanaoyafanya''.

Nasema: Wamefutu wajuzi katika vitabu vya fiqhi kwenye mlango waridda kuwa: Mwenye kutemka neno la ukafiri huwa kafiri na angatokusudia maana yake. Na hili linaonyesha kuwa wao hawajui hakika ya Uislamu, wala asli ya kupwekesha kwa hivyo wakawa ni makafiri ukafiri wa tangu mbele, kwani M'ngu amewalazimisha waja wake kumpwekesha kwa ibada. ''Kwamba musimuabudu ila M'ngu'' na kumtakasia yeye hio ibada ''Na wala hawakuamrishwa isipokuwa wamuabudu hali ya kumtakasia yeye dini'' — SURA: 98 Aya 5.

Na mwenye kumlingania M'ngu usiku, mchana kwa siri na dhahiri, kukhofu na kutumai kisha akamlingania pamoja na yeye mwengine, huwa kwa hakika ameshirikisha katika ibada, sababu dua ni katika ibada. Na hakika M'ngu ameiita dua ibada kwenye neno lake; ''Hakika wenye kufanya kibri na ibada yangu'' — SURA: 40 Aya 60 — baada ya kusema kwake: ''Niombeni mimi nitawatakabalia''.

Ukisema kuwa: Wakiwa niwashirikishaji italazimu kuwapiga jihadi na kwenda nawao mwendo alio kwenda Mtume kwa washirikishaji. Na kujibu: Kwenye (rai) hii wamekwenda mkao wa wamaimamu wa Ilmu, wakasema: Inapasa kuwaita wao kwenye kupwekesha (TAUHIID) na kuwabayinia kwamba: wanayo yaitakidi kufaa na kudhuru hayawatoshelezi wao kwa M'ngu, chochote, na

kwamba wao ni kama hao (washirikishaji), na kwamba (itikadi yao hii kwa hao ni shirki, hakutimu kuamini walio kuja nayo mitume ila kwa kuyawacha na kwa kutubu nayo, na kwa kupwekesha umoja wa M'ngu — KWA KUAMINI NA KUFANYA — kwa M'ngu pekeyake, na huu niwajibu juu ya wanavyoni, yaani: kubayini itikadi kwamba itikadi hio ambayo kumetokamana nayo kueka manadhiri, na kuchinja vichinjwa, na kutufu makaburi: (itikadi hio) ni shirki ilioharamu, na kwambayo ni ile ile waliokuwa wakiifanya washirikishaji kwa masanamu yao. Wanavyoni wakisha kubayini hilo kwa viongozi na wafalme, itawalazimu viongozi na wafalme kupeleka walinganizi kwa watu kuwaita wao kwenye kutakasa umoja wa M'NGU. (Hapo) mwenye kurudi na akakiri atajihifadhia damu yake na mali yake na watoto wake. Na mwenye kupindana, M'ngu atahalalisha kwake kile alicho muhalalishia Mtume (S.A.W.) kwa washirikishaji.

Ukisema: Kutaka kuokolewa kumethubutu katika hadithi. Kwani imesihi kwamba waja siku ya kiyama watataka kuokolewa kwa Adamu baba wa wanadamu kisha kwa Ibrahimu, kisha kwa Musa. Kisha kwa Isa, na watakomea kwa Muhammad (S.A.W.) baada ya kuliona zito (jambo hilo) kil'a mmoja katika mitume. Basi hii ni dalili juu ya kwamba kutaka kuokolewa kwa asiekuwa M'ngu si munkar.

Nasema: Huu ni udanganyifu! Kwani kutaka kuokolewa kwa walio hayi juu ya jambo wanaloliweza hakukatai yoyote. Na hakika M'ngu amesema, katika kisa cha Musa pamoja na Muis-raili na Mkibti, kwamba:

"AKAMUOMBA YEYE AMUOKOWE, YULE AMBAYE NI KATIKA JAMAA ZAKE JUU YA YULE AMBAYE NI KATIKA ADUI ZAKE" — SURA: 28 Aya 15.

Na hakika yalipo maneno ni katika kutaka kuokolewa watu wa makaburi na wengineo kwa mawaliyi wao na kutaka kwao kwa wao mambo (ambayo) hayawezi asiekuwa M'ngu Mtukufu: kama afiya ya mgonjwa, na mengineyo!

Kwamwe ajabu kuliko hili: ni kwamba hawa watu wa makaburi na wasiokuwa wao katika walio hayi miongoni mwawafuasi wawenye kuwaitakidi wanawapa baadhi ya watoto wa kipona na wananunua kwa wanae muitakidi mimba katika tumbo la mama ili ipate kuishi, na wanaleta maovu ambayo washirikishaji wa kwanza hawakuyafikia.

Na hakika walinambia baadhi ya wenye kushikilia upokeaji wa nadhiri zenye kuwekwa na watu wa makaburi, kwa baadhi ya makaburi kwamba: "Mtu mmoja alikuja na mapesa na mapambo ya wake zake, na akasema: (MALI) haya ni ya bwana wake fulani akusudia mwenye kaburi — (haya) ni nusu ya mahari ya binti yangu, kwa sababu ni memuoza na nilikuwa nime M'milikisha, fulani (mwenye kaburi) nusu yake.

Hizi nadhiri za mali, na kufanya fungu nila kaburi, wanavyo fanya kitu fulani katika makulima wanacho kiita (TALAM) katika baadhi ya pande za Yaman, ni jambo ambalo hawakulifikia waliokuwa wakiabudu masanamu, nalo linaingia kwenye neno lake M'ngu:

"NAWANAVIPA WA SIVYO VIJUA FUNGU KATIKA TULIZO WA RUZUKU" pasina shaka wala ruba — SURA: 16 Aya 56.

Ndio! kuomba kuokolewa waja siku ya kiyama na kutaka kwao kwa mitume (HILO), ni kumuomba M'ngu mtukufu aamue baina ya waja kwa hisabu iliawapunguzie wao vituko vya msimamo huo, na hili halinashaka kufaa. Na kusudia kuombeana M'ngu, hawakuwaombea hawa, kamwe Mtume alimwambia Umar alipotoka (Umar) kwenda kufanya (Umra): "USITUSAHAU NDUGU YANGU KATIKA DUA ZAKO".

Na M'ngu ametuamrisha kuwaombea waumini na kuwatakia maghufira katika neno lake: "Ewe mola wetu tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa kuamini" — SURA: 59 Aya 10.

Na ummu saliym (R.A.) alisema: "Ewe mtume wa M'ngu khadimu yako ANAS muombee M'ngu".

Na hakika masahaba (R.A.) walikuwa wanomba dua kwake mtume (S.A.W.) naye yu hayi, na hili ni jambo liloafikianwa kufaa kwake. Na maneno yako katika kutaka watu wa makaburi kwa miti au kwa walo hayi, ambao hawajimilikii nafuu wala dhara, wala kufa wala kupona wala kufufuliwa, (kuwaomba wao) wa waponye wagonjwa wao, wamregeshe alie potea wao, wamsahilishie mwenye mimba wao, wayanyweshelee makulima yao, wazibubujishe nacho zawanyama wao, na wahifadhi (nyama) na jicho, (la uhasidi) na kama hayo katika matakwa ambayo hayawezi ila M'ngu, hawa ndio ambao M'ngu amesema kuhusu wao: "Na hao mnao walingania asiekuwa M'ngu hawawezi kuwanusuru wala wenyewe hawajinusuru". SURA: 7 Aya 197. "Hakika mnao walingania niwaja kama nyinyi" SURA: 7 Aya 194).

Basi nivipi aombe, mwanadamu kwa kisichokuwa na roho au kwa kilicho hayi — ambacho kuwa na roho ni bora kuliko hicho — kwa kuwa hakina lazima? Na hili hubayini walilo lifanya washirikishaji ambao M'ngu alisimulia habari yao katika neno lake: "Na wamemfanyia M'ngu, katika alizo ziumba miongoni mwa makulima na wanyama, fungu wakasema: "HILI NI LA M'NGU WA MADAIYAO, NA HILI NI LAWASHIRIKISHWA WETU" SURA: 6 Aya 136.

Na amesema: "Na wanavifanyia wasiovijua fungu katika tulivyo waruzuku, na apa kwa M'ngu wataulizwa mno waliokuwa wakiyazua!" SURA: 16 Aya 56.

Hawa watu wa makaburi na wenye kuwaitakidi wajinga walio hayi na wapotevu wao wamefuata njia za washirikishaji kama zinavyo fuatana mbele za mshale, wakaitakidi kwao ambayo haifai kuyaitakidi ila kwa M'ngu; wakawapa wao fungu katika mali na wakayakusudia makaburi yao kutoka majumbani kwao yalio mbali kwa ajili ya kuzuru, na wakatufu makaburi yao, na wakasimama kwa unyenyekevu mbele ya makaburi yao na wakawalingania kwenye mashida, na wakachinja vichinjwa kwa ajili ya kujikurubisha kwao — na hizi ndizo sampuli zaibada tulizo kujulisha. Na wala sijui kuwa kuna kati yao mwenye kuwasujudia? Silioni mbali kupatikana kati mwao mwenye kufanya hivyo, kamwe amenieleza nnae muamini kuwa yeye amemuona mwenye kusujudu juu ya mlango waziyara ya waliyi anae mkusudia, kwa ajili ya kumtukuza na kuabudu, na wanaapa kwa majina yao.

Kamwe akiapa, anae lazimiwa na haki, kwa jina la M'ngu hawamkubalii, na akiapa kwa jina la waliyi katika mawaliyi wao wanamkubalia na wanamsadiki.

Na hivi ndivyo walivyokuwa wenye kuabudu masanamu.

"Na akitajwa mwenye ezi M'ngu peke yake zinakirihika nyoyo za watu ambao hawaamini Akhira na wakitajwa ambao ni asiekuwa yeye, mara wao wanafurahi" — SURA: 39 Aya 45.

Na ni katika hadithi swahihi: "Mwenye kuapa na ape kwa M'ngu au na nyamaze".

Na mtume (S.A.W.) alimsikia mtu akiapa kwa (LAT) (Sanamu) akamuamrisha yeye aseme: "LAILAHA ILLA LLAHU" na hili lina onyesha kuwa yeye aliritadi kwa kuapa kwa sanamu akamuamrisha yeye aujadidishe Uislamu wake. Kwani yeye alikufuru kwa hilo, kama tulivyo lithubutisha katika (SUBULIL-SSALAM SHEREHE YA BULUUGHUL-MARAM) na kwenye (MIN-HATUL-GHAFFAR).

> Ukisema: Sisawa kwani hawa wamesema:
>
> "LAILAHA ILLA LLWAHU" na mtume amesema:

"Nimeamrishwa nipigane na watu mpaka waseme: "LAILAHA ILLA LLWAHU", wakisema hivyo watazihifadhi nami damu zao na mali yao Illa kwa haki yake" na hawa wanaswali, wanafunga, na wanatoa zaka, na wana hiji kinyume na washirikishaji.

Nasema: Hakika mtume alisema: "illa kwa haki yake: nahaki yake ni kumpwekeshea M'ngu mtukufu uola na umja. Na hawa watu wa makaburi hawakupwekesha

uola na ibada. Kwa hivyo halikuwafaa wao neno la shahada, kwani hilo neno halifai illa likiwa pamoja na kujilazimisha maana yake. Kama ambavyo hakukuwafaa Mayahudi kulisema kwa sababu ya kukanusha kwao baadhi ya Mitume, na ni hivyo mwenye kumfanya asie kutumwa na M'ngu, kuwa ni mtume: halikumfaa yeye neno la shahada, huoni kuwa wana wa Hanifa walikuwa wakikubali kuwa hapana M'ngu illa (Allah), na kwamba Muhammad ni Mtume wake, na wakiswali, lakini wao walisema kuwa: "Musaylamah ni Mtume, masahaba wakapigana nao, na wakawatukana wao. Je vipi kwa anaempa waliyi yenye kumukhusu M'ngu na akamwita yeye Kwenye majambo ya muhimu?

Na huu ndie (Amiril muuminina) Aly bin Aby Twalibi (R.A.) aliwachoma jamaa wa Abdullah bin Sabai, na walikuwa wakisema: "Tuna kubali kuwa hapana M'ngu illa ALLAH na kwamba Muhammad ni Mtume wa M'ngu". Lakini walizidisha mno katika kumtukuza Aly (R.A.) na wakaitakidi kwake wanayo ya itakidi watu wa makaburi na kama wao, akawatesa wao mateso hakumtesa kwayo yoyote katika maasi, kwani aliwafukulia wao mashimo na akawarurumbishia moto akawatupia ndani na akasema:

*Mimi ninapoliona, lolote la munkari,*
*Na chochea moto sana, nikamwita kambari.*

Na akasema mshairi katika zama hizo:

*Mauti nayanitupe, yatakapo sitojali,*
*Bora mimi niyahepe, hayo mashimo mawili,*
*Chochelepo mahalipe, moto mkali kwa kweli,*
*Kufa kulikuwa kweli, ni taslimu sideni.*

Na kisa hichi kiko katika FAT-HUL-BARY na kisicho kuwacho katika vitabu vya hadithi, na sira.

Na hakika imepita Ijmaa ya umma kwamba mwenye kukanusha kufufuliwa huwa kafiri je vipi kwa mwenye kumfanyia M'ngu mwendani?

Ukisema: kuwa Mtume (S.A.W.) alimkemea Usamah kwa kumuuwa aliesema "LAILAHA ILLA LLWAHU" kama 'Hapana shaka kuwa mwenye kusema: "LAILAHA ILLA LLWAHU" katika makafiri anaihifadhi damu yake yake na mali yake, mpaka lidhihiri kwake lenye kukhalifu alilolisema, na kwa hivyo mwenye ezi M'ngu aliteremsha kukhusu kisa cha Mah-lam bin Jathamah aya: "Enyi watu mlio amini mkipiga katika njia ya M'ngu fafanueni" — SURA: 4 Aya 94. Kwa hivyo M'ngu akawaamrisha wa hakikishe kukhusu mwenye kunena neno la tauhidi. Akijilazimu maana yake atapata wanalo pata Waislamu na atapaswa na liwapasalo wao, na ikidhihiri kinyume nalo: hahifadhi damu yake na mali yake kwa kutemka tu.

Na kwa hivi killa mwenye kudhihirisha tauhidi, ni lazima kukomanae mpaka lidhihiri kwake lenye kukhalifu hilo. Likidhihiri halimfai hili neno tupu. Na kwa hivyo halikuwafaa Mayahudi, wala halikuwafaa (Khawariji) — pamoja na ibada walizokuwa nazo, ambazo masahaba walikuwa wakidharau ibada zao kulingana nazo.

Kamwe aliamrisha Mtume (S.A.W.) wauawe, na akasema: "Naapa nikiwawahi nitawauwa kama kumuuwa ADI".

Na hilo ni walipo khalifu baadhi ya sharia.

Na wakawa ni watu waovu mno chini ya Mbingu, kama zinavyo thubutisha hadithi!

Kwa hivyo imethubutu kwamba utupu waneno latauhidi hauzuii kuthubutu shirki ya alielisema kwa ajili ya kufanya lenye kulikhalifu, nako ni kuabudu asiekuwa M'ngu.

Ukisema: watu wa makaburi na wengineo katika wenye kuitakidi kwa mafasiki wa watu na wajinga wao kati ya walio hayi — wanasema: Sisi hatuwaabudu hawa, wala hatumuabudu asiekuwa M'ngu, wala hatuwaswalii wao, wala hatufungi, wala hatuhiji (kwa ajili yao). Nasema: Huko ni kutojua manna ya ibada; kwani ibada sio hayo tu ulioyataja, kwani kichwa cha ibada na msingi wake ni itikadi. Na hakika limepatikana katika nyoyo zao hilo. Kamwe wanaliita itikadi na wanamfanyia hayo ulioyasikia kati ya mambo yaliotokamana na kuamini: Kama kuwaomba, na kuwalingania, na kutawasali kwao, na kutaka kuokolewa na wao na kuwaomba msaada, na kuapa, na kuwawekea nadhiri, na yasiokuwa hayo.

Na hakika wametaja wanavyoni kwamba mwenye kujipamba kimakafiri huwa kafiri, na mwenye kutemka neno la kufuru huwa kafiri. Je, vipi kwa aliefikilia daraja hii ya kuitakidi, kusema, na kufanya?

Ukisema hizi nadhiri na vichinjwa ni nini hukumu yake? Nasema: Killa mwenye akili amejua kwamba: mali nikipenzi cha wenyewe, wanakwenda mbio kwa ajili ya kuyakusanya, japo ni kwa kufanya maasiya yote. Na wanakata masafa mengi karibu na mbali, yoyote hatoi chochote katika mali yake illa kwa kuamini kuvuta manufaa makubwa kuliko hicho, au kujiepusha madhara.

Mwenye kuiwekea kaburi nadhiri hatoi mali yake illa kwa ajili ya hilo. Na hii ni itikadi mbovu.

Na lau kama mwenye kueka nadhiri angejua makosa ya alilotakidi hangetoa hata derehemu.

Kwani mali nikipenzi cha wenyewe. M'ngu amesema: "Na wala hawaombi nyinyi mali zenu (yote) kama angewaomba (yote) akazidisha (katika kuyataka) mngefanya ubakhili na angetoa chukizenu" SURA: 47 Aya 6, 37. Wajibu ni kumjulisha mwenye kutoa nadhiri kwamba: ni kupoteza mali yake. Na kwamba hakimnufaishi yeye anachokitoa. Wala hakimuondolei madhara

Na hakika Mtume (S.A.W.) amesema: "Hakika nadhiri haileti kheri na hakika tu inatolewa kwa bakhili" na nilazima kumregeshea mwenyewe ama yule mwenye **kupokea nadhiri; (najue kwamba): Huko kupokea** nadhiri ni haramu juu yake kupokea, kwa sababu huko ni kula mali ya mwenye kueka nadhiri kwa batili sio kwa kupa chochote, na hakika M'ngu amesema: "Na wala musile mali yenu kati mwenu kwa batili" — SURA: Aya 188.

Kwa sababu huko ni kumthubutisha muekaji nadhiri juu ya shirki yake na uovu wa itikadi yake, na kuridhika kwake kwa hilo, na wala haifichamani hukumu ya mwenye kuridhia shirki.

shwa na anasamehe isiokuwa hio (shirki) kwa amtakae"
"Hakika mwenye ezi M'ngu hasamehe kushirikishwa na anasemehe isiokuwa hio (shirki) kwa amtakae" — SURA: 4 Aya 48.

Malipo hayo ni kama ada ya mkuhani na mahari ya umalaya, kwa sababu huko ni kumdanganya mwenye kueka nadhiri; na nikumfahamisha makosa kwamba waliyi anamfaa yeye na anamdhuru. Ni kuthubutisha makosa kupi kuliko kukubwa kuliko kupokea nadhiri ya maiti? Na niudanganyifu upi mkubwa na nikuridhika kupi kwa maasia kuliko kukubwa mno kuliko huku? Na nikufanya uovu kuwa wema kupi kunako ajabisha kuliko hili? Na hazikuwa nadhiri za masanamu ila juu ya mpango huu: anaamini mwenye kueka nadhiri kuvuta manufaa kwa sanamu na kuondoa Madhara, hapo akamuekea nadhiri sehemu kubwa ya mali yake na anagawanya naye zilo ndani ya udongo wake na akaja nacho mpaka kwa watumishi wa masanamu na wakakabidhi toka kwake na wakamfahamisha uhaki waitikadi yake, na uhaki wa kuleta kichinjwa chake na akakichinja mlangoni kwa sanamu, na hivi ndivyo vitendo ambavyo M'ngu aliwaleta mitume kwa ajili ya kuviondoa, na kuvifuta na kuviangamiza, na kuvikataza.

Ukisema: Mwenye kueka nadhiri henda akapata manufaa na akaondoa madhara kwa sababu ya kuitoa nadhiri na kuipa. Nasema: Na ni kama hivyo masanamu huenda likapatikana kwao kubwa kuliko hili, nalo ni maneno yenye kutoka ndani yao, na kuyaeleza anayoyaficha mwanadamu.

Ikiwa hii ni dalili juu ya uhaki wa makaburi na kusihi kuyaitakidi; na liwe basi ni dalili juu ya uhaki wa masanamu. Na huku ni kuuvunja Uislamu na kusimamisha nguzo za masanamu.

Na ukweli ni kwamba Iblisi na askari wake katika majini na wanadamu anamsaada mkubwa katika

miili, na kutia wasiwasi kwenye vifua na kumeza nyoyo kwa gorombo lake. Basi ni hivyo hivyo anaingia ndani ya masanamu, na akatia maneno katika masikio ya watu, na kama hilo analifanya kwenye itikadi za watu wa makaburi; kwani mwenye eziM'ngu amemruhusu avute kwa farasi wake na mguu wake wanadamu, na ashiri-kiane nao katika mali na watoto; Na limethubutu kwenye hadithi kwamba: "Shaytani anasikiliza kwa kuiba jambo ambalo M'ngu atalileta, na akalitupa kwa makuhani — na hao ni wale wenye kueleza khabari za ghaibu, na wanazidisha juu ya lile analolitupa shaytani mengi mengine mia ya uongo wao wenyewe".

Na wanakusudia mashaytani wakijini na wakibi-nadamu kwa watumishi wa makaburi na wangineo, wa-kiwambia:

"WALIYI AMEFANYA NA AMEFANYA"

Wanawapendezeshea wao na wanawahadharisha wao kukhusu yeye! Na utawaona jamaa, wafalme wa majimbo na watawala wamiji wakiyatukuza hayo, na wakiwaayini watumishi wenye kukabidhi nadhiri, na pengine wanalishikilia watu ambao watu wanawadhania wema; mwana chuoni, kadhi, au mufti, au sheikhe sufii, hapo ukatimu udanganyifu wa Iblisi na likatulia jicho lake kwa kudanganya huku.

Ukisema: Hili ni jambo limeenea miji, na wameku-sanyika juu yake wakaazi wamapango na majabali, na limewamba ardhi mashariki na magharibi, Yaman na Sham, kusini na Adeni, kwa namna ambao hupati mji katika miji ya Kiislamu illa huwa pana makaburi na mazi-yara na walio hayi wanaitakidiwa na kutukuzwa, na

kuekewa nadhiri, na kuitwa majina na kuapwa kwayo, na wanatufu milia ya makaburi, wanayawashia mataa, na wanayawekea mauwa na maraihani, na wanayavisha nguo, na wanafanya kila jambo wanaloliweza lakuyaabudu. Na ambayo yana maana ya ibada; ya kutukuza, kunyenyekea na kujidhalilisha na kuyahitajia, kamwe hii ndio misikiti ya waislamu, mingi kati yao haikosi kaburi au lilo karibu nayo au ziyara yenye kukusudiwa na wenye kusali katika nyakati za swala, wanafanya katikalo yote yaliotajwa, au baadhi ya yaliotajwa, wala haliikundukii akili ya mwenye akili kwamba hayo ni MUNKAR wenye kufikilia uovu ulio utaja, walio unyamalia wanavyoni ambao kumethubutu kwenda kwao pande zote za ulimwengu.

Nasema: Ukipenda ukweli na ukawacha kuwafuata wa kale, na ukajua kwamba haki ni ile tu ilio simama juu yake dalili, sio walioafikiana walimwengu kizazi baada ya kizazi, na mkao baada ya mkao, jua vile vile kwamba mambo haya ambayo tunakariri kuyakanusha, na twedambio ili mnara wake kuuangusha: (ni mambo) yenye kutokamana na wajinga ambao Uislamu wao ni wa kuiga wazee pasina dalili, na kufuata kwao huko ni kwa pasina kutafautisha kati ya twevu na yenye kufaa. mtu anainukia akawaona watu wakijiji chake na wenye mji wake wanamfunza udogoni aliite jina la wanaemuitakidi, na anawaona wakimuekea nadhiri, na wakimtukuza, na wakisafiri naye mpaka kwenye kaburi yake, na wanampaka yeye mchanga wake, na wanamtufisha juu ya kaburi hilo. Hapo (ndipo huyo mtoto) anainukia na hali umethubutu utukufu wa wanaemtukuza moyoni mwake, na huwa ashakuwa ni katika vitu vitukufu kwake huo wanae muitakidi, kwa hivyo anainukia

juu ya itikadi hii akiwa mdogo na anazeeka juu yake na wala hasikii ukemevu kutoka kwa yoyote juu yake. Kamwe unaweza kumuona, mwenye kusifika kwa ujuzi, na mwenye kujidai ubora, na anaeshikilia ukadhi, na kufutu, na kusomesha na utawala, au maarifa, au uamiri na sirikali, (utamuona) ni mwenye kuyatukuza wanayo yatukuza mwenye kuyakirimu wanayo yakirimu, mwenye kupokea nadhiri, mwenye kula vyenye kuchinjwa juu ya makaburi; hapo wainga wanadhania kwamba hii ndio dini ya Kiislamu, na kwamba hichi ndicho kichwa cha dini na nundu yake; na wala halifichamani kwa mwenye kufaa kufikiri, na anaejua un'gan'gaza wa ujuzi wa Kurani na hadithi . . . . kwamba kunyamaza mwanachuoni au ulimwengu juu ya kutuka MUNKAR si dalili ya kufaa MUNKAR HUO.

Na tupige mfano wa hilo nao ni hizi mukusi zenye kuitwa mujabi zenye kujulikana uharamu wake katika dini wazi. Zimejaa majumba na viwanda na zimekuwa ni jambo lenye kuzoewa, hakulipitii kulipinga, sikio lolote na mikono ya wenye kupokea mukusi imefika mpaka kwenye viwanda vitukufu, katika maka, mama wa miji wanapokea kwa wenye kuikusudia kwa ajili ya kutekeleza faradhi ya Uislamu, na wakakuta katika mji mtu
leza faradhi ya Uislamu, na wakakuta katika mji mtukufu mambo ya haramu, na hali wakazi wake ni katika bora wa viumbe, na wajuzi na mahakimu, wamenyamaza hawalikanyi wamelipa maungo kulileta na kulitoa.

Je, kunyamaza kutakuwa dalili juu ya uhalali wa kuzipokea na kuzihifadhi? Hili halisemi mwenye chembe ya kutambua. Kamwe na kupigia mfano mwegine: Hii ni haram ya M'ngu ambayo ndiyo bora wa viwanda

vya ulimwengu kwa itifaki na Ijmaa ya wanavyoni, wamezua katikayo (haram) baadhi ya wafalme waovu wajinga, upotevu: haya maqamu man'ne, ambayo yametenganisha ibada za waja na yakabeba mahaya ambayo hayadhabiti ila M'ngu mtukufu; yametenganisha ibada za Waislamu zikawafanya Waislamu ni kama wana mila tafauti kwenye dini, huo ni uzuzi (BID'A) uliolituza jicho la Iblisi mal'uni. Na yamewafanya Waislamu kama vicheko vya mashetwani; na watu wameyanyamazia; Na wanakuja (Maka) wana vyoni wapande nyingi na mabadal na makutbi, na ameyaona hayo killa mwenye macho na ameyasikia killa mwenye masikio; je, kutakuwa huku kunyamaza ni dalili ya kufaa mambo yenyewe?

Hili halisemi mwenye japo kitu kidogo katika maarifa! Ni kama kunyamaza kwao juu ya haya mambo yenye kutokamana na watu wa makaburi.

Ukisema: italazimu kuwa umma umekusanyika juu ya upotevu kwa kule kuwa wamenyamaza wasiukanye ujinga mkubwa.

Nasema: hakika ya Ijmaa: ni kuafikiana watu wa Ijtihad wa ummati Muhammad (S.A.W.) juu ya jambo baada ya zama zake Mtume; na wanavyoni wa madhehebu man'ne hawafai kujitahidi baada ya maimamu wa N'ne; Na lingawa hili ni neno labatili halisemi asiekuwa ambae ni mjinga wa hakika; Kwa madai yao: (Hapana Ijmai kabisa baada ya maimamu wan'ne) kwa hivyo haiji hio suali. Kwani uzuzi huu na kufitinika huku kwa makaburi hakukuwa katika zama za maimamu wan'ne.

Na kulingana na haya tunayo yahakikisha, huwakutuka Ijmaa ni muhali.

Kwani umati wa Muhammad (S.A.W.) umejaa pande, na umefika katika killa nchi na uko chini ya kulla nyota; Kwa hivyo wanavyoni wake wenye uhakika hawahisabiki, wala hapana anaeweza kujua hali zao. Kwa hivyo mwenye kudai Ijmai baada ya kuenea dini, na kuwa wengi wanavyoni waKiislamu; madai hayo ni ya uwongo, kama walivyo sema maimamu wenye kuhakikisha.

Kisha tukisema kwamba walijua Munkari na wasiukanye, kamwe walinyamaza, wasiukemee, kunyamaza kwao hakungeonyesha kufaa hilo (la Munkari). Kwani kunajulikana katika kawaida za sharia kwamba njia za kukanya ni tatu:

*Kwanza:* Kukanya kwa mkono; Nako ni kuubadilisha munkari na kuuondosha.

*Pili:* Kukanya kwa ulimi kukitowezekana kubadilisha.

*Tatu:* Kukanya kwa moyo ikitowezekana kubadilisha kwa mkono na ulimi.

Likikosekana hili halikosekani jengine. Na mfano wake, nikupita mtu katika wanavyoni wadini kwa mmoja wa wenye kupokea Mukusi wakati anapopokea mali ya wenye kudhulumiwa. Huyu mtu m'moja katika wanavyoni wadini hawezi kumbadilishia, huo mwenye kuchukuwa mali ya masikini, kwa mkono wala kwa ulimi, kwani atakuwa ni kicheko cha maasi hao, kwa hivvo sharti ya kukanya kwa njia mbili itakosekana, na patakuwa hapakubaki illa kukanya kwa moyo ambako ndiko dhaifu mno wa imani. Inampasa, mweye kumuona huo mwanachuoni amenyamaza hakukanya pamoja na kuona anachokichukuwa jabari huo, aamini kwamba kumem-

shinda kukanya kwa mkono na ulimi, na kwamba amekanya kwa moyo wake. Kwani kuwadhania Waislamu vyema ndivyo ipasavyo na kuwataawilia iwezekanavyo ndivyo ilivyo; Wenye kuingia haram tukufu na wenye kuona majengo hayo yakishetwani ambayo yametenganisha neno la dini, na yakazifanya mbali mbali swala za Waislamu, wanaudhuru kwakutoyakanya illa kwa moyo tu, kama wenye kuwapitia washikaji mukusi na watu wa makaburi.

Na hapa ndipo panapoonekana uharibifu wa liloendelea kwa maimanu hao wakuchukuwa dalili hizo — kusema kwao kwamba: lilituka na lisikanywe, kwa hivyo likawa lj'mai.

Na namna ya uharibifu huo ni kwamba:

Kusema kwao: "NA WALA LISIKANYWE" ni kutupa ovyo, kwani huenda ikawa nyoyo nyingi ziliona uzito kukanya mkono na ulimi. Wewe unashuhudia katika zama zako mambo mangapi yanatuka huyakanyi kwa ulimi wako wala kwa mkono wako, hali wewe unayakanya kwa moyo wako.

Na muinga anasema: akikuona unayaona; fulani amenyamaza hakuyakanya kwa neno lake, ama kwa kulaumu au kwa kuiga kule kunyamaza kimya hakuchukuliwi ni dalili na mjuzi yoyote.

Vile vile kunajulikana batilika neno lao katika kuchukuwa dalili: "FULANI AMEFANYA NA WENGINE WAMENYAMAZA" kwa hivyo ikawa Ijmai — (hili nalo) nilenye kubatilika kwa njia mbili:

*Kwanza:* kudai kwamba kunyamaza waliobakia huthubutisha kitendo cha fulani, kwa yale ulioyajua ya kunyamaza kutofaa kuwa dalili yenye kuthubutisha.

*Pili:* kusema kwao: "Ikawa Ijmai"

Kwani Ijmai ni kuafikiana ummati Muhammad (S.A.W.), na mwenye kunyamaza hanasibishiwi kuafiki wala kukhalifu, mpaka umbayini yeye ulimi wake.

Mfalme mmoja alisema: wakati watu katika hadhara yake wamemaliza kumsifu mtu mmoja katika wafanyi kazi wake, aliyekuwa kwenye hao watu, alikuwa amenyamaza! Mfalme akamuuliza: "Mbona wewe husemi chochote kama wanavyo sema?" Huyo mtu akajibu kwamba: "Nikisema nitawapinga". Basi sio kwamba killa kunyamaza ni kuridhia. Kwani haya ni maovu yalioasisiwa na mwenye upanga na mkuki mkononi, na damu za waja na mali yao yako chini ya ulimi wake na kalamu yake, na vyeo vyao viko chini ya kauli yake na neno lake; atawezaje Mtu M'moja kumpinga analolitaka?

Haya makuba na maziyara ambayo yamekuwa njia kubwa ya kwenda kwenye shirki na kutoamini; na chombo kikubwa cha kuuvunda Uislamu na kubomoa jengo lake, wengi au wote walio ya amirisha ni wafalme na masultani na wakuu na watawala, ima kumfanyia jamaa yao au kumfanyia wanae mdhania wema; M'bora, au mjuzi au Sufi, au fakiri au mzee au mkubwa. Na watu wakamzuru, ambao wanamjua, kama wanavyo zuriwa maiti pasina kutawasali kwake, wala kulilingania jina lake bali wana muombea M'ngu na kumtakia maghufira, mpaka wanapo ondoka wanaomjua au wengi katika wao.

wanakuja wengine baada ya hao wakaliona kaburi limejengewa, na limewashiwa mishumaa, na limetandikwa matandiko ya fakhri na limeteremshiwa mapazia, na limetupiwa mawaridi na mauwa, hapo wana amini kwamba (kaburi) hili nilakunufaisha au nilakudhuru; Na wakalijia watumishi wakimzulia maiti kwamba amefanya, na amefanya amemdhuru fulani amemfaa fulani mpaka wakameza kwenye moyo wa mwenye kusikia killa jambo la batili.

Na kwa hili imethubutu katika hadithi za Mtume: "Lana ni juu ya mwenye kuwasha taa juu ya makaburi na mwenye kuyaandika, na mwenye kuyajengea.

Na hadithi za hilo ni nyingi, zinajulikana. Kwani hilo lenyewe limekatazwa, kisha ni njia ya uharibifu mkubwa.

Ukisema: Hii ndio kaburi ya Mtume (S.A.W.) imejengewa kuba kubwa, lilotumiliwa mali mengi.

Nasema: Huu ni ujinga mkubwa kukhusu hakika ya jambo lenyewe; kwani hili kuba hali kujengwa nae Mtume (S.A.W.) wala na masahaba wake wala walio wafuatia wao na wala walio fuata waliofuatia, na wala siwanavyoni wa umma wake na wala siviongozi wa mila yake; Kamwe hili kuba lilojengwa juu ya kaburi ya Mtume (S.A.W.) ni katika majengo ya baadhi ya wafalme wa Misri waliokuja nyuma! Naye ni KALAWOONI L-SWALIHY. Anaejulikana, kwa jina la Al-malikul-mansoor. Katika mwaka wa 678 A.H. amelitaja hilo mwenye kitabu "TAH'KII KUL-NNUSRAH BITA KH'LIISWI MAALIMIL-HIJRAH".

Kwa hivyo haya ni mambo ya kidola sio ya kidalili, wa mwisho anamfuata wa kwanza!

Na hili ndilo mwisho watulilolitaka katika tulio ya leta zilipoenea beluwa na zikafuatwa "Hawaa" na wanavyoni wakapa maungo kukanya ambako kunawapasa, na wakapendukia walipo pendukia wajinga. Na uovu ukawa wema, na wema ukawa uovu. Wala asipatikane kwa watu mwenye kukataza hilo wala mwenye kukemea!

Ukisema: huafiki, kwa walio hayi na walio kufa, kukutana na watu wenye kufanya yenye kupasua ada, wenye alama za wenye kuvutika (majadhibi); Je ni nini hukmu ya hayo wanayoyafanya katika hayo mambo? Kwani hayo mambo nikati ya yenye kuvuta nyoyo ziyaitakidi hayo?

Nasema: Ama wenye alama za majadhibi, ambao wanalitafuna temko la utukufu (LAFDHUL-JALALAH) kwa vinywa vyao na wanao lisema kwa ndimi zao, wanao liepusha na temko lake lakiarabu: hao ni askari wa Iblisi mwenye laana, na ni katika ambao shetwani amewavisha mapambo ya udanganyifu na kuhadaa, kwa kule kuwa kulitupa neno la jalalah (Allah) mbali na kutimiziwa maneno kwa kusema kwao (Allah) (Allah) simaneno wala sitauhidi, kamwe ni kucheza na neno hili tukufu, kwa kulitoa nje ya temko lake la Kiarabu, kisha kuliepusha na maana yoyote!

Na lau kama mtu m'moja mtukufu mwema, anaitwa (Zayd), watu wakashikilia kusema Zayd, Zayd, Zayd angelichukuwa hilo kama shere na kutwezwa, na dharau: Na khaswa kukiliongezekea neno lenyewe temko lake.

(BADALA YA KUSEMA (ALLAH) WANASEMA: HA HAAN) Kisha angalia: Je. limekuja katika Kurani, na hadithi, temko hilo lajalala peke yake na likakaririwa?

Kwa sababu lilo kwenye Kurani na hadithi, ni kuamrishwa kumtaja M'ngu na kumpwekesha, na kuumsabbihi na kuhalili.

Na hizi ndizo dhikri za mtume (S.A.W.) na dua zake na dua za ali zake na masahaba wake zote hazina zivumi hizi na vitunu hivi na kelele hizi, ambazo wamezizoea ambao wako mbali mno na M'ngu na uongofu wa Mtume wa M'ngu (S.A.W.).

Kisha pengine wao wanaliongezea hilo jina tukufu majina ya jamaa fulani walio kufa, kama: IBNU ALWAN na Ahmad IBNUL-HUSEIN, na ABDUL-KADIR na AL-AYDARUSI.

Kamwe hali imefikia kuwa wanawakimbilia watu wa makaburi wanapodhulumiwa au wanapoonewa: Kama Aly Ruman, na Aly l-ahmar na kama hao.

Na hakika M'ngu amemuhifadhi Mtume (S.A.W.) na watu wanguo (Ah-lul-kisaa) na masahaba watukufu, hawakutiwa ndani ya vinywa vya wajinga hawa wapotevu, wenye kukusanya sampuli nyingi za ujinga na shirki na kufru.

Ukisema: Huenda yakaonekana mambo ya ajabu kwa hao wenye kulitafuna jina katika hao watu waupuzi na uhuni, na waonekana na mambo ambayo yanadhaniwa kuwa ni karama, kama kujichomeka kwa visu vikali, na

kama kuchukuwa majoka na visusuli (n'ge), na kula moto, na kuushika kwa mikono, na kutembea ndani ya moto kwa miili yao.

Nasema: Hizi ni hali za kishetwani, na wewe utakuwa mwenye kudanganyika ukiyadhania kuwa ni karama za hao maiti, au ni mema ya walio hayi, kuwa huo mpotevu alipoyaita majina yao aliwafanya ni washiriki wa M'ngu katika kuumba na kuamrisha; Hawa maiti ambao unawajaalia kuwa ni mawaliyi wa M'ngu, je, waliyi wa M'ngu anaridhia afanywe mshirika wa M'ngu na maj-dhubina na muasi?

Ukilidai hilo utakuwa umeleta jambo bovu mno, na umewafanya hao maiti ni washirikishaji na umewatoa, (M'ngu apishembali) nje ya duara ya Uislamu na dini: kwa kule kuwafanya wao ni wendani wa M'ngu, hali ya wao kuliridhia na kulifurahia, na itikadi kuwa hizo ni karama za majadhibi hao wapotevu tena washirikishaji, wenye kufuata killa batili; wenye kuzama ndani ya mabahari ya matwevu, ambao hawamsujudii M'ngu hata sijda moja, na wala hawamtaji peke yake!

Kwa hivyo ukilidai hili utakuwa umewathubutishia karama washirikishaji makafiri, na wenye wazimu; na utakuwa umevunja kwa hilo vidhibitisho vya Uislamu na misingi ya dini wazi na sharia yenye kunyoka sawa. Na ukisha jua ubatili wa mambo haya mawili huwa umejua kwamba hizo ni hali na ni vitendo vya kishetwani na niamali za ki Iblisi, wanazozifanya mashetwani kuwafanyia ndugu zao kwa ajili ya kusaidiana mpande mbili, kwani limethubutu katika hadithi kwamba mashetwani na majini wanajifanya kama majoka, na hili ni jambo

limekatiwa kutuka. Basi hao majoka anaowaona mwanadamu kwenye mikono ya majadhibi, huenda yakawa ni katika uganga, na uganga ni sampuli nyingi, na kujifundisha si tabu, kamwe mlango wake mkubwa ni kumkufuru M'ngu, kama kueka mswahafu choni na kama hayo!

Basi, nasihadaike mwenye kuona kubwa kwake mambo hayo ya majadhibi ambayo anayaona kuwa ni yenye kupita kawaida, kwani uganga una taathiri kubwa katika mambo.

Na vile vile wanavigeuza vitu kwa uganga na mengineo. Waganga wa Fir-auna, waliujaza wangwa kwa majoka mpaka Musa (A.S.) akaogopa. Na M'ngu (Mwenyewe) aliusifu kuwa ni uganga mkubwa. Na uganga unafanya kubwa kuliko hili. Ametaja IBNU BATUTA na asiekuwa yeye, kwamba yeye aliona bara Hindi watu wanawashiwa moto mkubwa wakavaa nguo nyembamba, na wakajichomeka kwenye moto huo, na wakatoka na nguo zao kama kwamba hazikuguswa na chochote!

Kamwe ametaja kwamba alimuona mtu, kwa mfalme M'moja wa bara Hindi, aliekuja na watoto wawili, kisha akawakata kipande kipande; kisha akatupa killa kipande upande wake mbalimbali, mpaka yoyote akawa haoni chochote katika vipande hivyo; kisha akapiga ukelele na akalia, hapo waliohudhuria hawakufahamu illa kuona killa kiungo kimeteremka chenyewe na kimeambata kiungo mwenzie, mpaka killa mtoto akawa hayi sawa sawa.

Amelitaja katika safari yake nayo ni safari fupi, nami nimefupiliza. Nilisoma Makka mwaka wa 1132

A.H. na akatuandikisha Mufti wa madhehebu ya hanafiyah katika MADINA Bw. Muhammad BIN AS'AD (M'ngu amrehemu). Na katika kitabu: "A-AGHANY" cha ABIL-FARAJ Al-AS-FIHANY kwa sanad yake: (iko) kwamba mganga m'moja alikuwa kwa Al-Waliid BIN UKBA huo mganga akawa anaingia ndani ya ng'ombe kisha anatoka. Bw. Jundub akamuona yeye hapo akarudi nyumbani na akabeba upanga wake, yule mganga alipoingia ndani ya ng'ombe Jundub, alisema: "MNALETA UGANGA HALI MNATIZAMA?" Kisha akampiga ng'ombe katikati, akamkata na akamkata huo mganga vilevile, watu wakababaika, hapo waliid akamfunga na akamuandikia Uthmani Bin Afaan kumweleza hayo; Na aliekuwa amesimama hapo jela ni mtu mmoja mnasara, alipomuona Jundub, anasimama (kwa ibada) usiku mzima, na mchana anafunga, alisema huo mnasara: "Na apa kwa M'ngu, watu ambao huyu ndie muovu wao ni watu wa ukweli": na hapo akamuakilisha mtu mwengine jola na akaingia (Mji) wa (KOFA); akauliza mwema wa wenyeji wake wakamuambia: ni Ash-ath Bin QAYS, akawa mgeni wake, hapo akamuona Ash-ath analala usiku na akiamka anataka chakula chake akatoka kwake na akauliza: "N'nani katika watu wa KOFA aliemwema zaidi?"

Wakamwambia ni JARIIR Bin ABDULLAH, akamkuta analala usiku na kukipambazuka anaagizia chakula chake. Hapo alielekea kibla na akasema: MOLA WANGU NI MOLA WA JUNDUB, NA DINI YANGU NI DINI YA JUNDUB na akasilimu.

Na Bayhaqii amekitoa kisa hichi katika Al-Ssunanil-kubraa pamoja na mabadiliko fulani katika kisa chenyewe. Ametaja mategemezewa yake mpaka kwa Al-as'-

wad, kwamba: Al-waliid bin Uqbah alikuwako Iraqi na mganga mmoja anacheza mbele yake; alikuwa anakata kichwa cha mtu kisha anampigia ukelele akasimama akipiga makelele hapo anamrudishia kichwa chake.

Watu wakasema: "SUB-HANA LLAHI" anawahuyi waliokufa, akamuona yeye mtu mmoja katika wema wa "MUHAJIRINA" ilipokuja siku ya pili alichukuwa upanga wake na akamkata kichwa chake, na akasema: "Akiwa ni mkweli najihuyi mwenyewe!" Al-waliid akamuamrisha Dinar mtu wa jela na akamfunga yeye, MW.

Kamwe ajabu zaidi kuliko hili: ni alilolitoa Albayhaqii kwa mategemezewa yake, katika kisa kirefu: Na kisa hicho, ni kwamba: Mwanamke M'moja alijifundisha uganga kwa malaika wale wawili WA BABILA, ambao ni HARUTA na MARUTA, na kwamba huo mwanamke alichukuwa ngano, akaiambia baada ya kuitupa chini: Jipande, nayo ikajipanda. Akaiambia: Jilime, nayo ikajilima, kisha akaiwacha; Halafu akaiambia: Jikaushe, nayo ikajikausha. Kisha akaiambia: Jisage, nayo ikajisaga. Mwisho akaiambia: Jifanye mkate nayo ikajifanya mkate. Akawa (huo mwanamke) hataki jambo illa linakuwa.

Na mambo ya kishetwani, hayahisabiki. Na yatosha atakayo kuyaleta DAJALI.

Na maagizo yake kwenye kufuata Kur-ani, na hadithi na kwenye kuzi khalifu. (KITABU KIMEKOMA HAPA)

رقم الإيداع : ٠٦٥٩ / ١٦

# تطهير الاعتقاد

عن

# أدران الإلحاد

تأليف

الإمام المحدث السلفي الشهير بالأمير

محمد بن اسماعيل اليمني الصنعاني

١٠٩٩هـ - ١١٨٢هـ

طبع ونشر

وزارة الشؤون الإسلامية والأوقاف والدعوة والإرشاد

وكالة شؤون المطبوعات والنشر

الرياض - المملكة العربية السعودية

وقف لله تعالى

١٤١٦ هـ

شركة ألوان للطباعة والصناعة المحدودة

ص . ب : ٦٤٦٣ الرياض ١١٤٤٢ ت : ٤٧٣٠٩٠١ فاكس: ٤٧٨٠٠٩٧